

**MWONGOZO WA JINSIA NA HAKI ZA WANAWAKE  
MAENEO YA SOKONI  
(BANDIKA KATIKA MAENEO YA BIASHARA NA  
SOKONI)**

**1. HAKI YA USALAMA WA MWILI: KUSHIKA SEHEMU ZA SIRI ZA MWILI AU VIUNGO VYA MTU BILA RIDHAA NI KOSA LA KISHERIA. TUNATETEA UHURU WA KILA MTU KUWA SALAMA NA KUHESHIMIWA MWILINI MWAKE.**

**2 EPUKA LUGHA ZA MATUSI NA UZALILISHAJI: LUGHA CHAFU, MATUSI, NA MANENO YANAYOZALILISHA HADHI YA MWANAMKE HAYANA NAFASI KATIKA JAMII YETU. ENDAPO IKITOKEA TO TAARIFA KUPITIA KIKUNDI CHA TIBA KILICHO KARIBU YAKO AMA OFISI YA UONGOZI WA SOKO ILI HATUA KALI ZA KISHERIA ZICHUKULIWE**

**3. HAKI YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA (WASH): KILA MWANAMKE ANA HAKI YA KUPATA MAJI SAFI NA SALAMA, KUTUMIA VYOO SAFI NA MIUNDOMBINU YENYE MAZINGIRA SAFI. TUTUNZE MAZINGIRA YETU KWA KUZINGATIA USAFI NA UTU WA WENGINE.**

**4. HESHIMA KWENYE BIASHARA ZA SOKONI: WANAWAKE WAJASIRIAMALI WANASTAHILI KUHESHIMIWA, SI KUDHALILISHWA..**

**5. UKATILI WA JINSIA NI KOSA KISHERIA: AINA YOYOTE YA UKATILI WA KIJINSIA NI KOSA KISHERIA, ENDAPO UTAKAMATWA HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO.**

**6. RUSHWA YA NGONO NI KOSA;KILA MWANAMKE ANA HAKI YA KUPATA HUDUMA PASIPO KUTOA RUSHWA**

**TUKOMESHE UKATILI WA KIJINSIA NA  
TUKEMEE TABIA ZA UDHALILISHAJI\*\***

